JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

***Anuani ya Simu "TAMISEMI" DODOMA***
***Simu Na: +255 26 2321607***
***Nukushi: +255 26 2322116***
***Barua pepe:ps@tamisemi.go.tz***

*Mji wa Serikali – Mtumba,*
*Mtaa wa TAMISEMI,*
*S.L.P. 1923,*
**41185 *DODOMA.***

Unapojibu tafadhali taja:-

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU AJIRA MPYA ZA WALIMU WA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI PAMOJA NA MAFUNDI SANIFU WA MAABARA

**Ndugu Wanahabari**,

Kama mtakavyokumbuka tarehe 07, Septemba 2020 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, alitoa kibali cha ajira mpya za Walimu 13,000 wa Shule za Msingi na Sekondari pamoja na Mafundi Sanifu wa Maabara za Shule.

Nachukua fursa hii kuwafahamisha kwamba taratibu za ajira tajwa kwa awamu ya kwanza zimekamilika ambapo Walimu waliokidhi vigezo wamepangiwa vituo vya kazi.

Walimu walioajiriwa ni wa fani zifuatazo:-

1. Walimu wa Shule za Msingi kwa mchanganuo ufuatao:-

   i. Walimu wa Daraja IIIA wenye Astashahada (Cheti) ya Ualimu;
   
   *ii.* Walimu wa Daraja IIIB wenye Stashahada (Diploma) ya Ualimu katika somo la *English* ***au*** aliyesomea *Elimu ya Awali;*

**iii.** Walimu wa Daraja la IIIC wenye Shahada ya Ualimu kwa masomo ya ***English, Civics, General Studies, History, Geography, na Kiswahili;***

iv. Walimu Daraja la IIIB na IIIC – waliohitimu Stashahada (Diploma) ya Ualimu (Elimu Maalum) kwa masomo ya ***Lugha***, ***Sanaa, Sayansi na Hisabati***;

**2. Walimu wa Shule za Sekondari kwa mchanganuo ufuatao:**

*i.* Walimu wa Daraja la IIIB wenye Stashahada (Diploma) ya Ualimu (Diploma) waliosomea masomo ya ***Physics, Mathematics, Biology, Chemistry, Home Economics na Agricultural Science;***

***ii.*** Walimu wa Daraja la IIIC wenye Shahada ya Ualimu waliosomea *Elimu Maalum* kwa masomo ya ***English Language, Geography, Physics na Mathematics;***

**iii.** Walimu wa Daraja la IIIC wenye Shahada ya Ualimu waliosomea masomo ya ***Physics, Mathematics, Chemistry na Biology;***

iv. Walimu wa Daraja la IIIC wenye Shahada ya Ualimu waliosomea masomo ya ***Agricultural Science, English Language, English Literature, Chinese, French, Book Keeping, Commerce, Accounts, Economics na Home Economics;***

v. Walimu wa Daraja IIIB waliohitimu Stashahada (Diploma) ya Ufundi;

vi. Walimu wa Daraja la IIIC waliohitimu Shahada ya Uhandisi katika fani ya Ujenzi, Umeme na Mitambo; na

vii. Mafundi Sanifu wa Maabara (Mafundi Mchundo) wahitimu wa Stashahada ya Ufundi Sanifu Maabara na Stashahada ya Sayansi na Teknolojia ya Maabara.

**Ndugu Wanahabari,**

Serikali imeweka kipaumbele kuajiri walimu kwa ajili ya Shule za Sekondari zenye michepuo ya Sayansi na Hisabari, Ufundi, Kilimo na Biashara, Maarifa ya Nyumbani (Home Economics), Lugha ya Kiingereza, Lugha ya Kichina na Lugha ya Kifaransa. Aidha, walimu wa masomo mengine wamepangwa katika vituo kulingana na upungufu uliopo ambapo kipaumbele ni Shule ambazo hazina kabisa walimu wa masomo husika. Kwa upande wa Shule za Msingi, upangaji wa walimu umefanyika kwa lengo la kuboresha uwiano wa walimu kwa wanafunzi. Kwa muktadha huo, Ofisi ya Rais -TAMISEMI imewapanga zaidi walimu wa Shule za Msingi katika shule za vijijini ambako ndiko kwenye upungufu mkubwa zaidi wa walimu.

**Ndugu Wanahabari**,

Napenda niwajulishe baadhi ya vigezo vilivyopewa kipaumbele katika kuchagua waajiriwa hawa ni pamoja na:-

i. Umri wa mwombaji usizidi miaka 45;
ii. Somo na kada ya ualimu aliosomea mwombaji ukilinganishwa na nafasi zilizotangazwa;
iii. Utimilifu wa nyaraka zilizotakiwa kuwasilishwa kwenye mfumo;
iv. Ulinganifu wa taarifa zilizopo kwenye vyeti na taarifa zilizojazwa kwenye mfumo;
v. Walimu waliomaliza Chuo kati ya mwaka 2014 na 2019;
vi. Uhalali wa nyaraka zilizowasilishwa;
vii. Waombaji waliochagua shule za mbali/vijijini ambazo hazina ushindani wamepangwa huko; na
viii. Pale ambapo waombaji wengi walikuwa na sifa zinazofanana, mfumo ulichagua mwombaji aliyetangulia kuomba.
ix. Aidha, katika ajira hizi mpya walimu wenye ulemavu wamepewa kipaumbele.

**Ndugu Wanahabari,**

Walimu waajiriwa wapya waliopangiwa vituo wanatakiwa kuripoti katika Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri zinazosimamia shule walizopangiwa na baadaye kwenye shule husika. Walimu hao wanatakiwa kuripoti katika Halmashauri walizopangiwa kuanzia tarehe **01, Desemba 2020** hadi **14, Desemba 2020** wakiwa na nyaraka zifuatazo:-

(i) Vyeti halisi vya taaluma vya Kidato cha Nne na Kidato cha Sita;
(ii) Vyeti halisi vya kitaaluma vya kuhitimu mafunzo ya ualimu ya ngazi husika;
(iii) Kitambulisho cha Taifa au namba ya utambulisho ya NIDA; na
(iv) Cheti halisi cha kuzaliwa.

**Ndugu Wanahabari,**

Napenda kutumia fursa hii kuwaelekeza waajiriwa wapya mambo yafuatayo:

i. Walimu waliopatiwa ajira waripoti na kufanya kazi kwenye vituo walivyopangiwa na kwamba vituo vyao vya kazi ni Shule za Msingi na Sekondari na sio katika Makao Makuu ya Halmashauri;
ii. Mwalimu au Fundi Sanifu wa Maabara atakayechukua posho ya kujikimu na baadaye asiripoti katika kituo chake cha kazi alichopangiwa atachukuliwa hatua stahiki kwa mujibu wa sheria ikiwa ni pamoja na kushitakiwa kwa kosa la kujipatia fedha/ mali kwa njia ya udanganyifu.;
iii. Wajiriwa wapya hawatabadilishiwa vituo vya kazi walivyopangiwa kwa kipindi cha miaka (3);
iv. Waajiriwa wapya wote wanatakiwa kujaza mikataba ya kutohama kwenye Halmashauri walizopangwa hadi baada ya kutimiza miaka mitatu (3) kwa waajiri wao; na

v. Waajiriwa wapya ambao hawataripoti katika vituo walivyopangiwa ndani ya siku 14 kuanzia tarehe 1 hadi tarehe 14 Desemba, 2020 watakuwa wamepoteza nafasi zao na nafasi zao zitajazwa na waombaji wengine wenye sifa waliopo kwenye Kanzidata (Database) ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

**Ndugu Wanahabari,**

Napenda kutumia fursa hii kuwaelekeza Wakurugenzi wa Halmashauri ambazo walimu hao wapya wamepangiwa kuwapokea na kuwawezesha kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya Utumishi wa Umma na baadaye kutoa taarifa ya kuripoti kwa walimu hao. Taarifa ya kuripoti waajiriwa hao zijazwe kwenye mfumo wa kielektroniki wa taarifa za Watumishi kwenye Tovuti ya Ofisi ya Rais- TAMISEMI baada ya kila mtumishi kupokelewa. Aidha, Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wanaelekezwa kukamilisha taratibu za ajira haraka ili walimu wapya waingizwe kwenye mfumo wa malipo ya mshahara (***Payroll***) mapema iwezekanavyo.

**Ndugu Wanahabari,**

Majina ya walimu waliopangiwa vituo vya kazi yanapatikana katika Tovuti ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI ya www.tamisemi.go.tz.

Asanteni kwa kunisikiliza.

**KATIBU MKUU**
**OFISI YA RAIS –TAMISEMI**
**27 Novemba, 2020**